



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

UTOAJI WA LESENI ZA MUDA MFUPI KIPINDI CHA MWISHO WA MWAKA

Dar es Salaam, 17 Desemba, 2024.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inatangaza fursa kwa wamiliki wa mabasi kuwasilisha maombi ya leseni za muda mfupi kwenye njia zenye uhitaji mkubwa wa huduma za usafiri wa abiria kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Leseni hizo zitatolewa kuanzia tarehe 17 Desemba, 2024 kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo;

- i) Basi liwe na uwezo wa kubeba abiria arobaini (40) au zaidi,
- ii) Basi liwe limefungwa kifaa cha kufuatilia mwenendo wa gari (VTD),
- iii) Basi liwe na Bima iliyo hai,
- iv) Basi likaguliwe na wakaguzi wa magari kutoka Jeshi la Polisi,
- v) Basi liwe na leseni hai ya LATRA,
- vi) Dereva awe amethibitishwa na LATRA, na
- vii) Basi liunganishwe kwenye Mfumo wa Tiketi Mtandao.

Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa utoaji leseni rrims.latra.go.tz nyaraka zifuatazo ziambatishwe;

- i) Nakala ya Kadi ya gari,
- ii) Nakala ya Hati ya Bima,
- iii) Nakala ya Ukaguzi wa gari kutoka Polisi,
- iv) Nakala ya Leseni ya Udereva.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia simu namba **0800110019** au **0800110020** au fika ofisi za LATRA zilizopo mikoa yote Tanzania Bara.

Salum Pazy
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano